**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI WA TARIME**

**TAREHE 02/12/2025**

# TANGAZO LA ZABUNI

## ZABUNI YA UPANGISHAJI VYUMBA VYA BIASHARA 10 KATIKA UWANJA WA SERENGETI, MTAA WA IGANANA

1. Halmashauri ya Mji Tarime inatarajia kumalizia ujenzi wa Vyumba 10 vya Biashara vilivyopo eneo la Uwanja wa Serengeti Mtaa wa Iganana Tarime Mjini, hivyo basi Halmashauri inawakaribisha mtu binafsi, Kampuni, Taasisi au kikundi kilichosajiriwa kisheria kwa ajili ya kupanga Chumba/Vyumba hivyo vya Biashara.

2. **Mwombaji unakaribishwa kuleta zabuni yako ya bei kwa ajili ya kuomba kupangishwa chumba cha Biashara,** kama ilivyo elekezwa kwenye fomu ya Zabuni na kama ilivyo fafanuliwa katika kipengele cha tatu cha tangazo hili. Vyumba vinavyo pangishwa ni **Chumba namba 65,66,68,81,82,83,87,88,89 na 91.** Mwombaji mwenye nia, utayari na uwezo anaweza kufanya ziara ya kutembelea na kukagua maeneo vilipo vyumba hivi kwa gharama zake muda wowote.

3 Fomu ya Zabuni itakuwa katika lugha ya Kishwahili na itanunuliwa na mwombaji anaehitaji kwa gharama ya **Tshs. 20,000/=** (elfu ishirini tu). Fedha hizo zilipwe Halmashauri ya Mji Tarime kupitia namaba ya malipo (Control number) utakayoipata katika ofisi ya Biashara namba 05 katika jengo la Halmashauri ya Mji Tarime. Fomu ya zabuni itatolewa Ofisi ya Manunuzi ofisi namba 44 saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kwa siku kwa siku za kazi.

4. Zabuni ijazwe kwa usahihi na iwe na nakala mbili zinazo fanana (2) (nakala halisi(Original) moja na nakala (copy) moja na kuwekwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa rakini na zitapokelewa kwenye sanduku la zabuni. Bahasha ziandikwe **ZABUNI KWA AJILI YA UPANGISHAJI (TAJA NAMBA YA KIBANDA) UWANJA WA SERENGETI)** na kuwasilishwa kwa mkono kwa anuani ifuatayo;

**Mkurugenzi,**
**Halmashauri ya Mji Tarime,**
**S.L.P 45,**
**TARIME**

5. Mwisho wa kuwasilisha zabuni ni siku ya Ijumaa tarehe 12/12/2025 saa 5:00 Asubuhi. Zabuni zote zitafunguliwa hadharani tarehe 12/12/2025 saa 5:00 asubuhi mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha mbele ya wawakilishi au waombaji walio amua kuhudhuria kikao cha ufunguzi katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji Tarime.

6. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya zabuni, zabuni za kielekroniki, na zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa zabuni kwa hali yoyote hazitakubaliwa kwa tathmini.

Imetolewa na

Gimbana Ntavyo
**MKURUGENZI WA MJI**
**TARIME**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA MJI WA
TARIME